# NINAKUABUDU MUNGU WANGU

Na. Abel T. Msigwa
DSM
August, 2021




2. Mafahamu yangu yadanganya, yanapokuona na kugusa,
Namsadiki Yesu hadanganyi, yeye Mungu Mwana na Ukweli.

3. Waficha Umungu, msalabani, na ubinadamu altareni,
Nami naungama zote mbili, kama mwivi yule mwenye toba.

4. Tho<u>mas</u> aligusa majeraha, nami nasadiki bila shaka,
Ewe Yesu nipe pendo lako, tumaini kwako na imani.

5. Umeteswa nini Bwana mwema, kwa kunipa mkate wa uzima,
Yesu unifiche ndani yako, ili nilionje pendo lako.

6. Yesu Pelikane nitazame, na kwa damu yako nitakase,
Tone moja ndilo linatosha, na dunia yote yaokoka.

7. Ndani ya mafumbo Yesu yumo, atafumbuliwa kwangu lini?
Nikuone Yesu uso wako, nishiriki nawe heri yako. AMINA.